



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA**  
(Barua zoteziandikwekwaMkurugenziMtendaji)



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb Na:KGR/BDC/S.2/28/137

03/08/2023

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi **04** za **Watendaji wa Vijiji Daraja III** kama inavyoonekana hapa chini:-

### **(1) WATENDAJI WA VIJIFI DARAJA III – (NAFASI 04) – TGS B**

#### **SIFA ZA MWOMBAJI.**

- Awe na Elimu ya Kidato cha IV au cha VI.
- Awe na Cheti cha Astashahada (**Technician Certificate – NTA LEVEL 5**) katika fani ya Utawala, Sheria, Maendeleo ya Jamii, Usimamizi wa Fedha au Sayansi ya Jamii kutoka Chuo Cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### **MAJUKUMU YA KAZI.**

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- Kuratibu na Kusimamia Upangaji wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kungeza uzalishaji mali.

Ajira yake itakuwa ya masharti ya kudumu na pensheni ya uzeeni.

**MASHARTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI.**

- Mwombaji awe ni raia wa Tanzania na mwenye umri usiozidi miaka 45.
- Mwombaji aambatishe nakala ya Cheti cha Kuzaliwa, Vyeti vya taaluma, Kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA maelezo Binafsi (CV), Vyeti vya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa wale waliofika kiwango hicho pamoja na Vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa. Hati za matokeo ya Kidato cha Nne na Sita (**Statement of Results**) havitakubalika.
- Picha moja Passport Size (**iandikwe kwa nyuma jina la mwombaji**).
- Wale ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma **Wasiombe Kazi** hii.
- Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe **kwa njia ya Posta** kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P 491,  
BUKOBA.**

Mwisho wa kutuma Maombi ni tarehe 17/08/2023.



Fatina Hussein Laay  
**MKURUGENZI MTENDAJI**

MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA  
HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA